# KATIKA KUTAFUTA AMANI

Kampeni zimefanyika mara kwa mara katika kila nchi kote duniani, huku viongozi wa nchi wa ngazi mbalimbali wakichaguliwa kushika nyadhifa zao. Na mara baada ya kushika madaraka yao, wananchi huanza malalamiko ya kutotimiziwa ahadi walizoahidiwa. Wapinzani huamka na kuanza kampeni zenye lengo la kuwatoa madarakani hao viongozi waliochaguliwa kwa kuwashutumu kwa uzembe na ukiukwaji wa haki. Viongozi waliochaguliwa nao huwashambulia wapinzani hao kwa madhumuni ya kutaka kuendelea na nyadhifa zao. Mapambano ya aina hii, matokeo yake ni maandamano ambayo pia yanaleta vita katika mitaa, uharibifu wa mali, vifo na kujeruhi wengi. Angalia kwa mfano katika Mashariki ya kati. Maelfu na mamia ya watu tayari wamekwishakufa huku wengine wakiendelea kufa kila siku kutokana na mapambano haya ya nguvu na kutokana na jitihada za kutaka kumiliki mali. Viongozi waliochaguliwa wanatumaini kwamba wanaongoza kwa amani na mafanikio. Malipo wanayoyapata ni milio ya risasi na milipuko ya mabomu yanayoyafanya makazi yao kuwa vifusi; na kukatisha maisha yao. Wale wanaobahatika kunusurika wanazikimbia nchi zao wakitafuta usalama wao katika nchi nyingine. Idadi kubwa ya watu hao ndio wale wanaozama baharini kabla hawajafika katika sehemu zile walizotamani kuzifikia ili kujificha huko.

Katika jitihada za kushika dola kwa nguvu, pindi mtu anapoendelea kufanya kinyume na matakwa ya wapiga kura, viongozi wa mataifa mengine huja kwa kuimarisha biashara zao huku wakipitia *{wakijificha}* katika uwanja wa kisiasa wa ulimwengu; lakini pamoja na hayo, kile wanachofaulu kufanya ni kuunganisha vikosi vya majeshi yao ili kulinda masilahi *{faida}* yao binafsi, na kwa njia hiyo husababisha mateso zaidi kwa wananchi wa eneo husika. Hii namna ya mipangilio ni maumivu juu ya maumivu, na kuongezeka kwa mapambano katika kiwango kinachoonekana sasa kuyaalika mataifa ya dunia yote kutengeneza makundi yasiyozuilika na yaliyo kinyume na makundi mengine kama hayo pia yaliyo katika mataifa mengine. Kwa hivyo basi; hali hii haiwezi kuleta amani; na badala yake, inaeneza machafuko tu ambayo hivi sasa yanaonekana kuelekea kuiambukiza dunia yote katika hali hii ya migogoro. Ni kitu gani kinafanyika? Ni kwa nini viongozi wanashindwa kuwapa wananchi yale ambayo kwa ajili yake waliwachagua?

## SIRI YA VIZAZI VYOTE

Viongozi hushika nyadhifa *{madaraka}* zao kwa kuahidi haki kwa kila mwananchi. Lakini baada ya kupewa majukumu yao ya kuelekea katika hiyo haki, kile kinachoinuka ni kukandamizwa kwa walio wengi. Wananchi nao huchukua hatua ya kuwatoa madarakani na kuwachagua wengine walioahidi kufanya vizuri zaidi. Lakini kwa jinsi inavyoonekana ni kwamba; hao viongozi wapya hufanya vibaya zaidi ya watangulizi wao! Hakuna hata uongozi mmoja katika taifa lo lote lile duniani uliofaulu kufanya kulingana na mahitaji *{au matakwa}* ya

watu wake wote kwa ujumla. Ni kwa nini? Je! yawezekana kuwa kuna upungufu wa ufahamu? Kwa nini wanadamu wameweza kufaulu kuboresha maswala ya Kiteknolojia vizuri kabisa, na kwa upande mwingine hali ya kijamii ikizidi kuzorota? Majibu ya maswali haya yanapatikana katika kitabu ambacho kinapatikana karibu katika kila familia, na karibu kila mahali watu wanakokwenda kufanya majukumu yao; lakini inaonekana ni wachache sana walioweza kukigundua! Je! ungependa kukitazama kitabu hicho na kupata majibu ndani yake? Ikiwa ndivyo; basi kichukue na ukifute vumbi na kisha tusome pamoja ili kupata majibu. Je! unajiuliza kuwa ni kitabu gani hicho? Naam; ni Biblia yako! Wakati mtengenezaji wa bidhaa anapotengeneza bidhaa mpya, huakikisha kwamba anaiambatanisha bidhaa hiyo na lebo yenye maelezo yanayoelezea kuhusu bidhaa hiyo kuwa ni nini hasa, na maelezo ya mwongozo wa namna ya kuitumia. Hali kadhalika; wakati Mungu alipowaumba wanadamu, aliwaambatanisha na lebo yenye maelezo yanayoelezea kuwa wao ni nini hasa, na ni jinsi gani wanaweza kuyaendesha maisha yao kwa njia rahisi na ya furaha na amani tele. Na lebo hiyo ni Biblia. Kwa hivyo basi; hebu na tuichukue na kuisoma ili tusikie Mungu anasema kuwa chanzo cha hii migogoro ni nini na nini pia tunapaswa kufanya ili kuitokomeza.

Akiwa muumbaji wa vitu vyote, na hakuna kinachoweza kukwepa maelekezo yake na kikafaulu; Mungu anaviona vyote, na hapa kwa mshangao anatuuliza swali akisema; ***"Vita vyatoka wapi, na mapigano yaliyoko kati yenu yatoka wapi?.." Yakobo 4:1.*** Tuna furaha kubwa kwa kuwa tunamzungumzia Mungu anayeogopwa na watu wote, ambaye hivi tunavyoongea, watu wote wakiwemo viongozi wanamwomba yeye kuleta umoja; yeye anayenena nasi katika biblia akiingilia kati ili kutuokoa na haya machafuko. Sasa basi tafadhalini; ikiwa kweli tunamaanisha kile tunachokiomba, hebu na tulifahamu jambo hili moja. Mungu anasaidia kwa kutoa mwongozo kwa ye yote aombaye na hivyo kwamba yule atakayetii; basi huyo ndiye atakayemwongoza kwa kumwelekeza namna ya kutoka katika tatizo hili. Maana Mungu anasema; ***"Mimi ni BWANA, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata. Laiti ungalisikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari" Isaya 48:17-18.***

Ni vyema kwamba tunaelekea mahali sahihi penye msaada. Lakini je! tuko tayari kusaidiwa? Kila nafsi na ijiulize swali hili. Na ikiwa tuko tayari; hebu basi twendelee na majibu ya Mungu huku kila mmoja akijichunguza sana moyo wake ili kuona ni kiasi gani amechangia haya matatizo, na kwamba sasa yuko tayari kiasi gani kufanya masahihisho. Tukiendelea na majibu ya Mungu wetu katika Yakobo 4, anasema; ***"…Si humu, katika tamaa zenu zifanyazo vita katika viungo*** *{mioyo}* ***vyenu. Mwatamani, wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi! Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya ili mvitumie kwa tamaa zenu" Yakobo 4:1-3.***

# NI KATIKA MOYO WAKO!

Je! unamwamini Mungu? Uko tayari kwa msaada wake wa majibu kwa sala zako? Basi kama uko tayari; anasema kwamba tatizo liko ndani ya moyo *{akili/nia}* wako! Kwa hivyo tafadhali elewa kwamba; hatua ya kwanza ya kutatua *{kusuluhisha}* tatizo ni kuacha mara moja kumnyoshea jirani yako kidole; na badala yake, ujinyooshee kidole wewe mwenyewe kwa kuitazama nafsi yako mwenyewe. Unaweza kushangaa na kujiuliza, **"nafsi yangu?!"** Ndiyo; ukweli ni kwamba, amini usiamini, lakini hapo *{ndani ya moyo wako}* ndipo tatizo lilipo! Uko tayari sasa? Kama jibu ni ndiyo; basi twendelee mbele ili tuone ni shida gani iliyomo ndani ya mioyo yetu.

Kama tulivyoanza kwa kusema; Sisi ni bidhaa ya Mungu, na ni yeye peke yake ndiye awezaye kutuambia kuwa sisi ni nini/nani hasa *{kwa msaada zaidi agiza ujumbe wetu usemao,* ***"MWANADAMU NI NANI?",*** *ili ujifunze zaidi; tutakutumia bure ujumbe huo}.* Tunajitahidi kufanya mambo pamoja ili kujenga mataifa yetu, na hata sayari hii dunia kwa ujumla. Lakini kila jitihada hukumbwa na mkwamo wa kutokubaliana kunakosababisha matengano na vita. Mungu anayathibitisha matatizo ya mioyo yetu, na kuonesha jinsi isivyowezekana kupata suluhisho la swala hili kwa kutumia mawazo ya mioyo yetu akisema; ***"…mwawezaje kunena mema, mkiwa wabaya? Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake. Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya" Mathayo 12:34-35.*** Na kwa hali hiyo basi; kwa vile kila jitihada zetu za kufanya mema huleta mabaya; basi lazima kwanza tukubali kwamba akili *{nia/ufahamu}* tunayotumia si sahihi, ina kasoro. Kumbukeni kwamba, ni vigumu *{haiwezekani}* kumsaidia mtu asiyekubali kuwa ana tatizo. Kwa hivyo kwamba inatuumiza kiasi gani; ikiwa tunahitaji msaada wa Mungu kwa kujibu maombi yetu, ni lazima kwanza tukubali kwamba tumekosea; maana kwa hakika, matendo yetu yasingeleta matokeo mabaya ikiwa sisi tuko sahihi. Sasa basi; tatizo letu ni nini?

Wakati Mungu yule tunayemwomba alipomaliza kumuumba Adamu, alimpa lebo yenye mwongozo wa maisha kwa njia ya mdomo *{yaani, kwa kuzungumza naye ana kwa ana; agiza ujumbe wetu usemao,* ***"MITI MIWILI",*** *kwa maelezo zaidi kuhusu hili},* lebo hiyo ndiyo ambayo baadaye kupitia kwa manabii na mitume iliandikwa na kuwa Biblia ambayo leo tunainukuu. Mara baada ya Mungu kumpa mwongozo, alimruhusu mwanadamu afanye uamuzi kuhusu kumfuata Mungu ama kumfuata Shetani. Kumbukeni wakati huo mwanadamu hakuwa mwovu wala mtakatifu. Ndipo alikuwa ameanza sifuri. Alikuwa tayari kuanza kama mtoto mchanga. Na kama sote tujuavyo; mwanadamu alichagua kumsikiliza Nyoka ambaye ni Shetani na Ibilisi ***{soma Ufunuo 12:9}.*** Ni kwa huo mwongozo wa Shetani ndio ambao mwanadamu alianzia, ndio unaomjaza elimu akilini mwake na kuitumia kama ufahamu wa kuyaendesha maisha. Kwa hivyo, ni kwa huo ufahamu *{elimu}* wa Shetani ndio ambao mwanadamu alianza kuutumia katika kuyaendesha maisha yake, na matokeo yake ndiyo haya machafuko tuyaonayo leo.

Kwa vile Shetani ni mwongo na mwuaji ***{soma Yohana 8:44};*** basi ni dhahiri kwamba, wanadamu walirithi uongo, maana Mungu analithibitisha hili akisema; ***"…Baba zenu hawakurithi kitu ila uongo, naam, ubatili na vitu visivyofaa. Je! mwanadamu ajifanyie miungu, wasio miungu?" Yeremia 16:19-20.*** Kwa kumweka Mungu na maagizo yake kando, mwanadamu alijifanya mwenyewe kuwa mungu pamoja na mali zake alizonazo, na kuanza kujitegemea mwenyewe. Lakini Muumba wetu anasema hatuwezi kuwa miungu. Naam; kwa kumwacha muumba wake, ambaye peke yake ndiye awezaye kuongoza katika njia ya kweli ya maisha; mwanadamu sasa anapambana na matokeo ya mwenendo wake mwenyewe, maana Mungu anasema; ***"Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema, Hatutaki kwenda katika njia hiyo" Yeremia6:16.*** Kwa hivyo wapendwa na ndugu wananchi; ni katika hii mioyo miovu ya ukaidi ndiko ambako vita hivi tunavyovishuhudia vinakotokea. Na kwa sababu hiyo basi; ***"Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika. Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele {****mwongozo wa maisha; soma* ***Mithali 3:1-3}. Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea, watu waliosalia wakawa wachache tu" Isaya 24:4-6.***

Baada ya kuukataa ukweli uhusuo maisha yetu, tumekwenda mbele zaidi na kusema kwamba, **"ni asili ya mwanadamu; ni mapenzi ya Mungu".** Eti mapenzi ya Mungu! Hakuna kilicho mbali na ukweli zaidi ya hili. Ni uchaguzi wetu mbaya ndio unaotuumiza, maana ndio tunaovuna matunda *{matokeo}* yake. Na kwa sababu hiyo; kadiri tutakavyoendelea na mioyo hii mibaya *{miovu}*, ndivyo ambavyo jitihada zetu pia zitakavyoendelea kuwa kazi bure, na kamwe ***"njia ya amani hatutaijua", soma Isaya 59:8.*** Hii ndiyo maana, pamoja na jitihada zote za Umoja wa Mataifa za kutaka kuleta amani na haki, zimeleta tu vita zaidi! Kwa sababu kile kitupasacho kufanya, na elimu ile tupaswayo kuitumia ambayo ni Neno la Mungu, tumeiweka kando *{tumeitupilia mbali}*. Kwa hivyo kwa kutokwenda katika njia iliyo sahihi; ***"Njia ya amani hawaijui; wala hapana hukumu ya haki katika miendo yao; wamejifanyizia njia zilizopotoka; kila apitaye katika njia hizo hajui amani. Kwa sababu hiyo hukumu ya haki i mbali nasi, wala haki haitufikilii; twatazamia nuru, na kumbe! Latokea giza; twatazamia mwanga, lakini twaenenda katika giza kuu. Twapapasa-papasa kutafuta ukuta kama kipofu, naam, twapapasa kama watu wasio na macho; twajikwaa wakati wa adhuhuri, kana kwamba ni wakati wa ukungu wa alfajiri; kati yao waliowanda tumekuwa kama wafu. Sisi sote twanguruma kama dubu; twaomboleza kama hua; twatazamia hukumu ya haki, lakini hapana; na wokovu, lakini u mbali nasi…Na hukumu imegeuka ikaenda nyuma, na haki inasimama mbali sana; maana kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia" Isaya 59:8-11,14.***

Wapendwa; je! maelezo haya ya biblia si hali halisi inayoikabili dunia na ambayo wanadamu wanajitahidi kutaka kuipatia ufumbuzi? Na sasa kwa kuwa Mungu ametuonesha

sababu na chanzo cha matatizo haya; je! tutaendelea na hizi jitihada zetu za bure, ama tuko tayari kubadilika?

## SULUHISHO

Kama tulivyotangulia kusema kwamba; ikiwa kweli tunamaanisha kile tukiombacho kwa Mungu; basi tutakubaliana naye kwamba tatizo liko kwa kila mmoja wetu katika namna *{njia}* yake ya kufikiria. Naam; tatizo liko katika mioyo *{akili/nia}* yetu. Unaweza kuwalaumu na kuwashutumu Wamarekani, Warusi, ama nchi jirani, ama makabila yanayokuzunguka, ama chama pinzani cha kisiasa, jirani yako, mume ama mke wako, ama ye yote yule unayeweza kumlaumu kwa kasoro hizi ama matatizo haya. Lakini yote hayo ni kazi bure! Mtu mmoja msomi alikuwa na maneno haya ya kusema pindi walipokuwa wakijadili namna ya kutatua matatizo haya haya tunayoyajadili hapa, wakiwa katika mkutano wa Umoja wa Mataifa. Alisema; *"Ni katika mioyo ya wanadamu ndimo ambamo vita hutengenezwa. Kwa hivyo pia ni humo humo katika mioyo ya wanadamu ndimo ambamo ujenzi wa amani unapaswa kuanzia. Cha kufanya ili kubadili mwenendo wa tabia hizi, ni lazima kwanza kubadili namna {njia} ya kufikiri"*. Bila shaka mtu huyu alirejea katika lebo ya mwongozo, maana alinukuu maneno yale yale ya ***Yakobo 4:1-3.*** Sasa basi; je! kweli tunahitaji ufumbuzi *{suluhisho}?* Je! tunahitaji amani katika familia zetu? Je! tunahitaji amani na umoja katika miungano *{jumuiya}* yetu? Je! sisi pamoja na viongozi wetu tunahitaji mbinu za kuelekea katika kujenga taifa lenye umoja? Kama jibu ni ndiyo; basi ni lazima *{tunatumia neno "lazima" kwa sababu hakuna njia nyingine mbadala. Kwa hiyo tunapaswa kuitumia njia hii, la sivyo tuzidi kupotea na kuangamia katika machafuko}* kila mmoja aanze kwa kujitazama mwenyewe ndani ya nafsi yake; na kujishughulisha kwanza na nafsi yake kabla ya kumfikiria mtu mwingine, kwa sababu kila mmoja ana tatizo la kushughulikia, maana Mungu anasema; ***"Wote wamepotoka, wameoza wote pia; Hakuna mtenda mema, la! hata mmoja" Warumi 3:12.***

Yesu, mjumbe aliyetumwa na Mungu kutuletea ufahamu wa lebo hii ya mwongozo alisisitizia pointi hii akiuliza; ***"mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako" Mathayo 7:3-5.***

Hapa tulipo wapendwa; Mungu amesikia kilio chetu, na yuko hapa kujibu maombi yetu. Anataka tuishi maisha ya amani, furaha na mafanikio. Kwa hivyo hebu basi tuanze kwa kuziondoa tofauti zetu ili kama tuombavyo, tuje katika taifa lenye umoja na amani. Hebu kila mmoja na achukulie kwamba yuko peke yake, na aanze kutatua *{kusuluhisha}* tatizo lake. Kubali kwamba ulikuwa ukitumia ufahamu *{nia/akili}* mbaya, maana Mungu anasema kwamba sisi sote tumepotoka. Tulipotea njia baada ya kumsikiliza Shetani ***"audanganyaye ulimwengu wote {Ufunuo 12:9}",*** ambaye hivi sasa ana furaha kubwa kwa sababu anauona udanganyifu wake ukituletea uharibifu. Naam; kubali kwamba kile tulichotumia kama ufahamu kilikuwa ni ujinga.

Tumefika katika ngazi ya juu katika kujifunza; katika shahada mbalimbali za Uprofesa n.k. Lakini tutakubaliana kwamba walio mstari wa mbele katika kuchangia hii migogoro ya dunia ni wasomi, maprofesa wenye PhD. Ni kwa nini basi usomi wao hauwawezeshi kutatua matatizo ya kijamii? Kwa sababu Mungu amethibitisha wazi kwa neno lake kwamba ufahamu huu ni wa kimwili tu; lakini kiakili na kijamii ni ujinga, maana anasema; ***"…hekima ya dunia hii ni upuzi mbele za Mungu",*** na kwamba, ***"mawazo ya wenye hekima ni ya ubatili", soma 1 Wakorintho 3:19-20.*** Je! tunamaanisha kwamba usomi *{elimu}* ni mbaya? La, hasha! Tusinukuliwe vibaya tafadhalini. Pointi ni kwamba; ni ujinga wa kutoyajua makusudi *{malengo}* halisi ya maisha, na kutafuta yaliyo tofauti; yaani wanadamu pamoja na kupiga hatua kubwa Kiteknolojia, wameitumia vibaya elimu hiyo na wameshindwa kufikia tamaa yao ya kuwa na hali ya amani na umoja.

Ni kidonge kichungu, lakini kama tunahitaji kufaulu katika hizi jitihada, hatuna uchaguzi mwingine zaidi ya kukimeza tu! Chukulia kwamba tumeukubali ukweli huu na tuko tayari kutembea kwao; hebu kila mmoja wetu aendelee na nafsi yake. Ili mtu afaulu katika kile anachotaka kufanya, ni lazima atumie kanuni za ufaulu. Kanuni ya kwanza na iliyo kuu ya ufaulu ni kuweka lengo *{goli}*. Na lengo letu hapa ni kupata amani na mafanikio katika ulimwengu wa umoja na ushirikiano. Hatutaweza kulifikia lengo kama hatuyafahamu madhumuni ya maisha yetu.

## LENGO SAHIHI

Kati ya mambo yasababishayo mapambano na mapigano mengi ni pamoja na jitihada za kutafuta utajiri pamoja na nafasi za heshima zinazokubalika katika jamii zetu. Tunadhania kwamba tukiwa navyo tutakuwa tumeyakamilisha maisha na hivyo kwamba tutaishi maisha marefu na ya amani. Lakini pamoja na kuwa navyo vyote, ***"wanakufa na kuwaachia wengine mali zao. Makaburi ni nyumba zao,..hao waliotaja mashamba yao kwa majina yao wenyewe…Hiyo ndiyo njia yao, ujinga wao, Nao walioko baada yao huyarithi maneno yao".*** Tena, ***"….kuna mtu ambaye kazi yake ni kwa hekima, na kwa maarifa, na kwa ustadi; naye atamwachia mtu asiyeshughulika nayo kuwa sehemu*** *{urithi}* ***yake…Kwa kuwa siku zake zote ni masikitiko, na kazi yake ni huzuni; naam, hata usiku moyoni mwake hamna raha…", soma Zaburi 49:10-11,13; Mhubiri 2:21,23.***

Naam; kile ambacho watu wanajaribu kukifikia kama lengo lao la maisha halitatui *{halisuluhishi}* matatizo haya tunayoyazungumzia; kumaanisha kwamba, hilo nalo ni tatizo! Kwa hivyo basi; liweke hilo *{lengo la awali}* kando, na tumrudie Muumba wetu, katika lebo ya mwongozo wa maisha *{yaani, Biblia}* aliyotupatia ili tupate kufahamu lengo sahihi. Na mwongozo huo wa maisha unatuambia kwamba, madhumuni ya maisha ni ***"kumcha Mungu, na kuzishika amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu" Mhubiri 12:13.*** Kwa maana nyingine ni kwamba; tuliumbwa katika miili hii ya damu na nyama ili kuishi kwa njia ile asemayo Mungu katika amri zake. Na hivyo kwamba tunatafuta utajiri, au amani, au umoja, naam; kutafuta ufanisi wa maisha; tunapaswa kwenda kwa mpango wa Mungu *{kwa maelezo*

*zaidi kuhusu hili, agiza kitabu chetu kisemacho,* ***"AMRI KUMI",*** *ili ujifunze zaidi; na tutakutumia bure kitabu hicho}.* Tunachokisema hapa ni kwamba; njia sahihi ya maisha ni ile ambayo amri za Mungu zinaifafanua; maana, ***"…ni uhai kwa wale wazipatao, Na afya ya mwili wao wote" Mithali 4:22.*** Lakini je! ni hili tu ndilo tupaswalo kufanya, yaani kuishi kwa maagizo ya Mungu? Ndiyo; sisi ni bidhaa ya mtengenezaji aitwaye Mungu. Alikuwa na madhumuni *{makusudi}* ya kutuumba sisi. Ikiwa tunahitaji kuishi maisha ya amani na ushirikiano, ni lazima tufuate kile asemacho. Lakini ni kwa kusudi gani? Dhumuni ni hili hapa; tafadhali lielewe ukiwa tayari kuelewa. ***"Mungu akasema, Na tumfanye mtu*** *{si Wakristo peke yao kama ambavyo wengi wanadhania, bali ni kuwafanya watu wote}* ***kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale…juu ya nchi" Mwanzo 1:26.***

Kumbukeni kile tulichosema awali kwamba; mwanadamu hakuumbwa akiwa mtakatifu wala mwovu. Alikuwa aanze kwa kupata ufahamu wa maisha kutoka kwingineko. Hatuzaliwi na huu ufahamu. Akili ya mwanadamu haizalishi *{haitengenezi}* ufahamu yenyewe; bali inategemea kupata ufahamu kutoka kwingineko kwa njia ya kujifunza. Lakini tulianza kwa kupata ufahamu mbaya, usio sahihi. Na kama tulivyoona; kile tukitumiacho sasa kama ufahamu ni uongo. Malengo yote tunayoyaweka katika jitihada za kuyaboresha mataifa yetu yamejengwa juu ya ufahamu mbaya. Lakini Mungu yuko hapa kutufunulia na kutuonesha lengo sahihi. Na kufikia hapa; tunapaswa kwenda katika kanuni ya pili ya ufaulu ama ufanisi. Kwa kuwa kanuni ya kwanza ni kuwa na lengo *{na lengo letu ni kupata amani na mafanikio};* basi tunahitaji kwenda mbele zaidi ili kulifikia lengo letu. Na ili tufaulu, tunahitaji elimu; ambayo ndiyo kanuni ya pili ya ufanisi; na hapa ndipo kujifunza Biblia *{yaani, kusoma lebo ya mwongozo wa maisha}* kunahitajika. Ni lazima sasa tujifunze upya kutoka katika chanzo sahihi cha ufahamu ili kupata maelekezo sahihi ya namna ya kuishi. Ndiyo kile Mungu asemacho kuwa kinatupasa kufanya katika haya maisha. Kwa nini? Ili tuwe kama Mungu, ni lazima tujifunze kuishi kama yeye; naye anaishi kwa njia ile aliyoifafanua *{aliyoielezea}* katika amri zake.

## ASILI YA MWANADAMU

Sasa tunakuja katika siri iliyojificha ya uasi na ambayo ni sababu kuu ya uovu wote. Tumefunuliwa lengo letu jipya ambalo linatuambia kwamba tuliumbwa ili tuwe kama Mungu, kwa madhumuni ya kuitawala dunia hii kama sehemu ya ufalme wake. Lakini ili tufanye hivyo *{yaani, ili tuitawale dunia kama sehemu ya ufalme wa Mungu},* tunahitajika kwanza kufanana naye kwa njia ya kujifunza kutoka kwake, na ndiyo kile tunachokwenda kufanya sasa. Bali Shetani alitudanganya. Alituambia kuwa tayari sisi tuko kama Mungu, tuna ufahamu mkamilifu, na hatuwezi kufa; maana alimwambia mama yetu Hawa kuwa Mungu ni mwongo, ***"…hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo*** *{wa ujuzi wa mema na mabaya},* ***mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya*** *{yaani, mkiwa na ufahamu wa kutofautisha au kupambanua mema na mabaya pasipo kutumia mwongozo wa Mungu}", soma* **Mwanzo 3:4-6.**

Naam; Shetani alimdanganya mwanadamu *{na mpaka sasa wanadamu wanatumia huo udanganyifu wake}* kwamba akili yake inaweza kutengeneza ufahamu yenyewe kwa namna ile ile kama Mungu alivyo. Kwamba akili ya mwanadamu inaweza kujiwekea sheria zake yenyewe kama vile Mungu alivyoweka na kujitengenezea maisha mazuri kama ya Mungu. Hapo ndipo tulipoutelekeza mwongozo *{yaani, Biblia}*, na kuanza kudhania kila kitu tukifanyacho na kuanza kuishi kwa njia hii tuishiyo kwayo leo. Na hii ndiyo maana, kuanzia kwa viongozi wetu mpaka kwa wale wanaoongozwa; na kuanzia kwa Umoja wa Mataifa mpaka katika ngazi za kifamilia; hatuoni wanadamu wakiwa makini *{wakichukulia kwa uzito}* katika kusoma Biblia ili kufahamu ni nini cha kufanya katika kila jambo maishani. Badala yake; kila taifa kupitia kwa dhana zake, limejiandikia mwongozo wake lenyewe *{yaani, Katiba ya nchi}.* Ndiyo kile wanachotumia kama mwongozo katika namna ya kutawala, kuhukumu na hata namna ya kufanya mambo yote kwa ujumla.

Tunaona pia kila familia ikiwa na mfumo wake wa maisha unaotegemeana na kile wakipendacho wenyewe. Mfumo huu wa uendeshaji wa mambo umeanzisha kile kiitwacho **"Ustaarabu",** na ndiyo kile tunachokiita kama **"Asili ya mwanadamu",** ambayo kiuhalisia ni **"Asili ya Shetani".** Na kwa kuwa nia ya Mungu ilikuwa ni kumfanya mwanadamu kuwa mtawala baada ya kuwa amemfanana *{kitendo kinachowezeshwa kwa kujifunza kwanza njia ya Mungu ambayo wanadamu waliipuuza}*, na sasa mwanadamu aliukubali uongo kuwa tayari yuko kama Mungu; basi kwa kuufuata uongo huo, wanadamu wakaanza kujitengenezea mataifa kulingana na dhana *{fikira/mawazo}* zao wenyewe; naye Mungu akawaruhusu, maana anasema; ***"…zamani zilizopita*** *{Mungu}* ***aliwaacha mataifa yote waende katika njia zao wenyewe" Matendo 14:16.*** *{Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu hili, agiza ujumbe wetu usemao,* ***"HUYU NI SHETANI",*** *ili ijifunze zaidi; tutakutumia bure ujumbe huo}.* Naam; wanadamu ***"…akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa*** *{wametenganishwa}* ***na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga*** *{uongo}* ***uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao*** *{kuukataa mwongozo wa maisha};* ***ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani" Waefeso 4:18-19.***

Kumbuka kwamba; hili ni jawabu la sala yako kutoka kwa Muumba wako. Anazungumza na wanadamu wote na wa namna zote za maisha. Ujumbe huu si kwa ajili ya wale walio na dini tu. Bali ni ujumbe wa Mungu kwa wanadamu wote uhusuo Amani kwa wote na ni kwa namna gani amani hiyo itapatikana. Hivi sasa tunayaona mataifa mbalimbali na huku mengine yakiendelea kutengenezwa *{kuanzishwa}.* Tunayaona mataifa tofauti yenye mila, tamaduni na desturi tofauti pia. Lakini ndani yao, tunaona kila moja likijifanya lenyewe kuwa **"mungu";** naam, lisiloweza kutaniwa ama kuchezewa; ndilo kubwa ama hodari zaidi; imara zaidi, lenye uwezo zaidi n.k. Hebu na tuwaambieni. Kwa vyo vyote vile tuwezavyo; ikiwa ni kwa ufahamu huu tunahitaji kutatua *{kusuluhisha}* tatizo hili; basi na tusahau kabisa kuhusu ukweli na uwazi, haki na usawa, heshima, ushirika na amani. Na hii ni kwa sababu; baada ya kuukataa ukweli pekee utokao kwa Muumba wetu, sifa hizi za maisha hazimo kabisa ndani yetu; maana Mungu anasema, ***"Miguu yao hukimbilia mayai, nao hufanya haraka kumwaga damu***

***isiyo na hatia; mawazo yao ni mawazo ya uovu; ukiwa na uharibifu zaonekana katika njia kuu zao…Na hukumu imegeuka ikaenda nyuma, na haki inasimama mbali sana; maana kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia. Naam, kweli imepunguka kabisa, na yeye auachaye uovu ajifanya kuwa mateka…" Isaya 59:7,14-15.***

Kwa hivyo kwa kutokuwa na sifa hizi za maisha wanayoyatamani, na kwa kila taifa kudhania kwamba litaifanya dunia yote kulifuata kwa lazima *{kwa kuyashurutisha kwa nguvu};* vita vimesambaa kila mahali, na vitazidi kuongezeka zaidi kwa kila taifa kutokubali kulegeza msimamo wake kwa sababu lenyewe ni mungu *{ni mungu kwa mujibu wa udanganyifu wa Shetani}.* Hili ni jambo la hakika kama kuchomoza kwa jua hapo kesho. Tunamaanisha kwamba; kama ilivyo lazima kwamba kesho jua litachomoza, ndivyo ilivyo pia kwamba, watu kuendelea na ufahamu huu mbaya wa awali, kamwe hawataweza kutatua matatizo yao.

Enyi viongozi; msipoteze muda wenu kwa kuwalaumu mnaowaongoza, na kuwakandamiza kwa kuwaingiza katika mateso katika jitihada zenu za kutaka kuwafanya wawaelewe. Matatizo yamo ndani yenu ninyi wenyewe. Nanyi mnaoongozwa; msipoteze muda wenu kwa kuwalaumu viongozi wenu na kujihusisha na maandamano yasiyo na mwisho na mapambano katika mitaa kama jitihada za kuwafanya viongozi wenu waone maana ama wapate hisia zenu. Matatizo yamo ndani yenu ninyi wenyewe. Nchi washirika; hebu msipoteze muda kwa kuwalaumu kabila fulani, wala chama pinzani cha kisiasa. Matatizo yamo ndani ya kila mmoja wenu. Na kama hatukubaliani na hili ambalo Mungu anatueleza hapa; basi tusipoteze muda wetu kwa kumwomba atupe amani na mafanikio, maana hana jibu lingine tofauti na hili unalolisoma katika ujumbe huu.

## SERIKALI MOJA YA DUNIA

Baada ya kujitahidi kupambana na matatizo ya kijamii yasiyosuluhishika pamoja na matatizo ya kuichumi, kila taifa linaonekana kukubali kwamba haliwezi kuyafanya mambo hayo peke yake. Umoja wa Ulaya umekuja na mbinu za pamoja kuhusiana na matatizo ya waamiaji watokao katika nchi zenye vita. Mataifa yanashauriana na mataifa mengine ili kubuni mbinu za pamoja za kuleta maendeleo. Miungano inaundwa ili kukabiliana na mashambulizi ya kigaidi. Hivi sasa, kuna hili wazo kwamba suluhisho la matatizo ya dunia hii ni kuwa na serikali moja ya dunia yenye katiba moja, soko la pamoja, jeshi moja, na mpango wa pamoja wa kijamii. Je! hili linawezekana? Ili jambo hili lifanyike; tunahitaji umoja wa akili mpya *{nia moja}.* Lakini hivi sasa, ianzie kwa kila mmoja, katika kila familia, kisha kwa kila kabila, taifa, ukanda; kama vile ambavyo hivi sasa wana akili *{nia}* tofauti. Na kila mmoja/upande unaamini kwamba akili zao ndizo pekee ambazo zikitumiwa zinaweza kuleta maisha mazuri wanayoyatamani. Naam; kama tulivyoona; wote wameufuata uongo ambao umezijaza akili zao, kiasi kwamba wamefanyika kuwa huo. Kwa hivyo je! inawezekana dunia kuja pamoja na kutengeneza serikali moja inayotawala dunia yote? Kile wanachofaulu kufanya ni kutumia mfumo wa utawala wa kutumia nguvu zao za kimwili kuwashurutisha wengine kufanya matakwa yao, na hivyo kuwaweka chini ya matakwa yao. Matokeo yake je? Kila taifa hivi sasa tunapouandika ujumbe huu, linakumbwa

na msuguano wa aina moja ama nyingine, na ambao ki ukweli unalisumbua sana. Kisha mara kwa mara, kila kiongozi wa nchi huondoka nchini kwake na kwenda kukutana katika mkutano wa Umoja wa Mataifa kwa lengo la kujadili namna ya kuleta amani na ushirikiano duniani. Huku pia wakitafuta namna ya kuwa na serikali moja. Lakini je! tunamaanisha hayo kweli? Ni kwa njia gani sisi ambao nchi zetu zina vita na tumeshindwa kuzisaidia, tunakusanyika kutengeneza njia ya amani ya pamoja? Ikiwa tumeshindwa kutatua matatizo yetu katika nchi zetu wenyewe; tutafanyaje basi pindi tunapokuja pamoja na huku kila mmoja akija na mawazo yake yaliyoshindwa kuleta ufanisi nchini kwake?

Wapendwa; kama tusipobadilika na kutoka katika akili hii tuliyonayo sasa *{ambayo imethibitika kutoweza cho chote};* basi kile tutakachojiletea hivi karibuni kama ufanisi wetu ni kutoweka kwa uhai wote katika Sayari hii dunia. Kwa kila taifa kulinda msimamo wake; na kuweka jitihada zao zote katika kutaka kuwatawala wengine; *"mataifa yanainuka kupigana na mataifa mengine {na kwa kuundwa kwa mipaka ya kimataifa, hivi karibuni kutawezesha} ufalme kupigana na ufalme…kusalitiana baina yao kunafanyika, makabila dhidi ya makabila**", soma Mathayo 24:7-10.*** Hii itakaribia kuleta vita vya tatu vya dunia. Na katika ulimwengu wa leo wenye silaha za maangamizi makubwa, na kwa kila taifa ama mipaka ya kimataifa wasivyokubali kulegeza misimamo *{itikadi}* yao, basi vita vikubwa vitaendelea kutokea. Na watatumia silaha hizi za maangamizi, pasipo kujali athari zake na kufanya ukiwa mkubwa. Hebu sikia kile Bwana wetu asemacho kuhusiana na athari za vita vitakavyopiganwa hivi karibuni *{na dalili zake ambazo tunazishuhudia hivi sasa ni katika nchi ya Siria na sehemu nyinginezo za dunia}.* ***"Moto*** *{yaani, mabomu}* ***unakula mbele yao; na nyuma yao miali ya moto inateketeza;*** *{kabla ya mashambulizi}* ***hiyo nchi inafanana na bustani ya Adeni mbele yao, na nyuma yao*** *{yaani, baada ya mashambulizi}* ***imekuwa jangwa tupu; naam, hakuna aliyeokoka asipatikane nao" Yoeli 2:3.***

Kwa hakika, tuna macho lakini hatuoni! Je! hii si hali halisi ya nchi zote ambazo vita vinapiganwa ndani yake? Lakini hata hivyo; vita hivi vinavyopiganwa hivi sasa ni cha mtoto vikilinganishwa na vile vijavyo! Hatuzungumzi ovyo; bali tunayanukuu haya kutoka katika lebo ya mwongozo wa maisha aliyoitoa Muumba wako kuhusu kile ambacho akili *{nia/mioyo}* zetu mbaya zitatuletea kama tusipobadilika. Mungu yuko hapa hivi sasa akituambia jinsi ambavyo akili zetu mbaya zitakavyotuendesha kutoka katika mabaya na kwenda katika mabaya zaidi! Akielezea matumizi ya ndege za kivita na hali ya mioyo ya watu; anaseam, ***"Kama mshindo wa magari ya vita*** *{mashine pekee za kivita zilizojulikana katika kipindi cha nabii Yoeli}* ***juu ya vilele vya milima, ndivyo*** *{ndege za kivita leo, zikiwemo zile zirukazo bila rubani}* ***warukavyo; kama mshindo wa miali ya moto ilapo mabua makavu, kama mashujaa waliopangwa tayari kwa vita. Mbele yao watu wanahangaika; nyuso zote zimegeuka kuwa nyeupe kwa hofu" Yoeli 2:5-6.***

Jihadharini na manabii wa uongo wanaokuja wakihubiri amani pasipo mabadiliko ya akili *{nia/mioyo}* yaletayo amani kama vile Muumba wetu asemavyo. Sheria ile ifanyayo kazi ndani yetu hivi sasa, ndiyo isababishayo maovu haya yote. Kwa hivyo, tusipoondoa chanzo; madhara

yataendelea kuonekana tu! Tunaiona hii tabia ya kuitana na kukusanyika pamoja kwa ajili ya maombi *{katika matamasha makubwa, na hata kufanya mkesha unaosindikizwa na burudani za kwaya mbalimbali},* lakini pasipokuwa na nia ya kutaka kubadili njia zetu. Na kisha manabii wa uongo husimama na kuhubiri amani. Lakini, ***"BWANA asema hivi katika habari za manabii wanaowakosesha watu wangu; hao waumao kwa meno yao, na kulia, Amani; na mtu awaye yote asiyetia kitu vinywani mwao, wao humwandalia vita" Mika 3:5.***

Kwa hivyo mpendwa; usidanganyike. Hebu sikiliza kile ambacho Muumba wako *{ambaye ndiye pekee akufahamuye vyema}* anakuambia leo hii na umtii yeye. Ujumbe huu ni wito wa uamsho kwa kila mwanadamu atakayependa kubadilika na kupata amani hata katika kipindi hiki cha fujo. Fahamu na tambua kwamba; wacha-Mungu wa kweli ni nadra *{adimu/wachache}* sana katika ulimwengu wa leo; idadi kubwa ya wale tuwaonao ni manabii wa uongo. Maana, ***"Mtu amchaye Mungu ametoweka, asionekane katika nchi, wala hapana mtu mwenye adili katika wanadamu; wote huotea ili kumwaga damu; kila mtu humwinda ndugu yake kwa wavu. Mikono yao inayashika mabaya wayatende kwa bidii; mtu mkuu aomba rushwa, kadhi yu tayari kuipokea; mtu mkubwa hunena madhara yaliyomo rohoni mwake; hivyo ndivyo wayafumavyo hayo pamoja. Mtu aliye mwema miongoni mwao ni kama mbigili; mtu aliye mwenye adili miongoni mwao ni mbaya kuliko boma la michongoma…sasa kutatokea kufadhaika kwao" Mika 7:2-4.*** Kama tusipojitoa ufahamu kwa kutaka kuufumbia macho uhalisia huu; basi wote tunakubaliana kwamba hii ndiyo hali halisi ya watu katika ulimwengu wa leo.

## MWISHOWE AMANI

Ikiwa haya tuliyoyaeleza hapa ndiyo sababu; je! ni kumaanisha kwamba Mungu ameachana na mpango wake kwa wanadamu, kwa kuona jinsi wasivyokuwa na nia ya kutaka kubadilika? Je! atawaruhusu wafuate njia hii ya uharibifu na kuyateketeza maisha yao wenyewe pamoja na uhai wote katika dunia kwa ujumla?

Takriban miaka elfu mbili iliyopita, Muumba wetu alimtuma mjumbe wake kama tulivyoanzia kuona katika ujumbe wetu huu mwanzoni, aliyeleta habari njema ambayo ndiyo tumaini pekee kwa wanadamu. Mjumbe huyo si mwingine, bali ni Yesu Kristo ambaye mpaka sasa, karibia ulimwengu wote unamdharau, na ujumbe wake pia wameukataa kama tulivyosema. Katika ujinga wetu, tutaendelea kushiriki katika njia hii ya uharibifu mpaka pale ambapo kila mmoja wetu atafikia mahali pa kukata tamaa. Hivi sasa, kila kiongozi pamoja na wasomi kadhalika, wote wanahofia hali ya dunia ambayo ni matokeo ya njia yetu mbaya ya maisha. Karibia kila kitu kinakwenda ndivyo sivyo *{kinakwenda mrama};* magonjwa yasiyotibika, matukio ya majanga, vita visivyokoma n.k. Mungu ametuambia wazi kuhusu kipindi hiki cha kukata tamaa akisema; ***"Kwa maana, tazama, Bwana, BWANA wa majeshi, atawaondolea…tegemeo lote la chakula na tegemeo lote la maji; mtu hodari na mtu wa vita; mwamuzi na nabii; mpiga ramli na mzee; jemadari aliye juu ya watu hamsini, na mtu mstahifu, na mshauri, na fundi aliye mstadi, na mganga ajuaye uganga sana*** *{na hapa,*

*akizungumzia kuhusu hekima na uwezo kutoweka katika watu; anasema}* ***Nami nitawapa watoto kuwamiliki, na watoto wachanga kuwatawala. Nao watu wataonewa, kila mtu na mwenziwe, na kila mtu na jirani yake; mtoto atajiinua mbele ya mzee, na mtu mnyonge mbele ya mtu mwenye heshima" Isaya 3:1-5.***

Je! hatuyashuhudii mambo haya yakifanyika katika jamii zetu? Viongozi wa leo wanatawala katika mazingira magumu sana kwa sababu wanaowaongoza hawana tena heshima kwao. Wazee nao karibia wote hawana nafasi katika jamii kwa sababu vijana hawawajali tena. Vita vimefikia mahali ambapo makamanda wakuu hawawezi tena kuvimudu. Tazameni jinsi ambavyo mataifa makuu yasivyoweza kuzuia hata mgogoro mmoja! Wanajitahidi kupambana pasipo matumaini. Itafikia kipindi ambacho watakata tamaa kabisa; naam; kipindi ambacho ***"…mashujaa wao wanalia nje, wajumbe wa amani wanalia kwa uchungu" Isaya 33:7.*** Kwa nini? Kwa sababu kila kitu kitakwenda ndivyo sivyo *{ama kitakwenda mrama},* na kile wakionacho kuwa kimesalia mbele yao, ni uharibifu juu ya uharibifu; maana, ***"Njia kuu zimeachwa, msafiri amekoma*** *{kwa kuhofia usalama}****;..Nchi inaomboleza, na kulegea;..imetahayarika na kunyauka…imekuwa kama jangwa…" Isaya 33:8-9.*** Kumbukeni; mambo haya yanakuja wakati ambapo wanadamu wanazidisha ugumu wa mioyo *{nia}* yao miovu, na kutokuwa tayari kuachana na mwenendo wao huo hata kidogo! Hii ndiyo sababu viongozi pamoja na wajumbe wa amani *{wasuluhishi}* wanalia kwa kuwa hawajui ni nini cha kufanya, na kwa wakati huo huo wanakiona kile kijacho mbele yao *{yaani, matumizi ya silaha za maangamizi}.* Na kufikia katika hatua hiyo; Mungu wa mbinguni, Muumba wa vitu vyote, ataingilia kati. Kama tulivyoona; hivi sasa, kila kiongozi *{raisi}* na waziri anatamani kuwepo kwa serikali moja ya dunia, ambayo wameshindwa kuitengeneza; na ambayo ndiyo pekee iwezayo kutatua *{kusuluhisha}* matatizo yaliyopo sasa katika jamii. Kwa hivyo kufikia hapo; Mungu wa mbinguni ameahidi kuingilia kati; maana anasema, ***"Basi, sasa nitasimama; asema BWANA; sasa nitajiinua, sasa nitajitukuza" Isaya 33:10.*** Na tena; ***"Tazameni, Bwana Mungu atakuja kama shujaa, Na mkono wake ndio utakaomtawalia; Tazameni, thawabu yake i pamoja naye, Na ijara yake i mbele zake" Isaya 40:10.***

Kwa hivyo wapendwa; ni huko kuingilia kati kwa Mungu kwa mamlaka *{mkono wenye nguvu}* ndiko kutakakozuia huu ukaidi wa wanadamu. Katika ujumbe wake; Kristo aliahidi kipindi hicho cha matumaini akisema; ***"Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni*** *{geukeni},* ***na kuiamini Injili*** *{mkaiamini habari hii njema ya ujio wa ufalme huo}****" Marko 1:15.*** Naam; kile kilichotamanika; yaani serikali moja ya dunia, inakuja; wakati ambapo wanadamu watakubali kubadili njia zao za kufikiri; maana, ***"Miisho yote ya dunia itakumbuka, Na watu watamrejea BWANA…" Zaburi 22:27.*** Je! watu watakumbuka nini? Sisi wa Kanisa la Mungu, hivi sasa twawaambieni chanzo cha maovu haya tuyaonayo leo na namna ya kuyatatua; bali wengi wenu hamtuamini kabisa! Lakini wakati huo utakapofika, Mungu ***"…atauharibu uso wa sitara*** *{upofu wa fikira}* ***iliyowekwa juu ya watu wote*** *{upofu unaowafanya hivi sasa wasielewe; soma 2 Wakorintho 4:3-4},* ***na utaji ule uliotandwa juu ya mataifa yote" Isaya 25:7.*** Mara jambo hilo litakapofanyika, ndipo watu wote watayakumbuka haya tuwaambiayo hivi sasa,

na ***“...Jamaa zote za mataifa watamsujudia. Maana ufalme una BWANA, Naye ndiye awatawalaye mataifa” Zaburi 22:27-28.*** *{Agiza ujumbe wetu usemao,* ***“HUYU NI SHETANI”****, pamoja na ule usemao,* ***“UFALME WA MBINGUNI”,*** *kwa maelezo ya msaada zaidi; nasi tutakutumia bure ili ujifunze zaidi}.* Ni ufalme huo ndio utakaokomesha vita hivi tunavyovishuhudia leo; maana punde tu utakaposimamishwa, watu ***“…watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu*** *{yaani, silaha zote za vita zitaharibiwa na kufanywa kuwa zana za kilimo};* ***taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe” Isaya 2:4.*** Naam; ***“Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima*** *{ufalme}* ***wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari” Isaya 11:9.***

Hata hivyo kabla ya wakati huo kufika; Mungu hivi sasa anaahidi ulinzi kwa kila mmoja atakayeusikia wito huu na kubadilika; maana anaahidi akisema; ***“Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi” Ufunuo 3:10.*** Tena; ***“Malaika wa BWANA hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao*** *{wanaoitii sauti yake}* ***na kuwaokoa…BWANA atakulinda na mabaya yote, Atakulinda nafsi yako. BWANA atakulinda utokapo na uingiapo, Tangu sasa na hata milele” Zaburi 34:7; 121:7-8.***

Hii ndiyo habari njema *{yaani, Injili}* tunayoitangaza kwa watu wote, na ambayo ndiyo tumaini pekee la amani na furaha. Je! waweza kuwa miongoni mwa wale wanaoyatazamia maisha hayo kwa dhati? Basi usifadhaike tena; maana Mungu amekuja kukulinda kwa kukutumia ujumbe wake huu. Kile unachopaswa kufanya ni kujiunga nasi kwa lo lote lile utakalohitaji kuhusiana na njia hii ya amani na furaha. Huduma yetu inatolewa bure kabisa kwako pasipo malipo utakayotozwa. Pia tambueni kwamba; mafundisho yetu yote ni mafundisho halisi ya Biblia, na wala si mafundisho ya kimadhehebu ya kidini kama ilivyozoeleka. Kwa hivyo mtu wa dhehebu lo lote lile *{na hata asiyekuwa na dini},* maadamu tu aiamini Biblia kama Maandiko *{sauti}* ya Mungu kwa wanadamu; awe huru kujifunza pamoja nasi.

Tunayo majarida yenye mada mbalimbali kama vile; “NI WAPI PA KUANZIA?, JE! WEWE NI MKRISTO?, KUOKOLEWA KWA NEEMA, THAMANI YA UKRISTO, SHETANI NI NANI?, ROHO YA SABATO ZA BWANA, HUYU NI SHETANI, MNYAMA WA UFUNUO, KANISA LA SIKU ZA MWISHO, KWA NINI SHERIA?, NI KANISA MOJA TU!, UBATIZO, TAFUTENI HESHIMA” n.k.

Pia tunavyo vitabu kama vile; “UFALME WA MBINGUNI, SIKUKUU ZA MUNGU, AMRI KUMI, KIFO NA KIYAMA, DINI ZA MITINDO, BIBLIA NA AFYA ZETU” n.k. Agiza vile utakavyohitaji; nasi tutakutumia bure kabisa na kwa gharama zetu wenyewe hadi mahali ulipo wewe.

Basi wasiliana nasi kwa anuani zetu hapa chini:

**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Idara ya uandishi na usambazaji** – MWANZA

Simu: +255 753 359 179, +255 688 359 179 & +255 655 659 179.

Barua pepe: Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg

**Idara ya usambazaji:**

MARA, - Simu: +255 755 409 202.

ARUSHA, - Simu: +255 754 028 574 & +255 782 422 216.

DAR ES SALAAM, - Simu: +255 762 055 056 & +255 672 611 204.

**KANISA LA MUNGU – KENYA**

Barua pepe: endcog@gmail.com

***Neema, rehema na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo ziwe pamoja nanyi. Utukufu na uweza una yeye tangu milele, sasa na hata milele; Amina.***